



LOWELL PUBLIC SCHOOLS
Henry J. Mroz Central Administration Offices
(Ofisi za Usimamizi wa Kati)
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

Novemba 2, 2020

Wapenzi Wanafunzi, Wafanyikazi, Familia na Wanajamii wa Lowell Public Schools,

Mwaka uliyopita, wilaya yetu ilichukuwa hatua muhimu katika mchakato wetu wa kupanga wa kimkakati kwa kufafanua kujitolea wetu wa kimsingi kwa usawa kama msingi wa kila sehemu ya kazi yetu. Lakini, tunajua kwamba maneno bila hatua hayana maana. Tunajua pia kwamba kama wakuu wa shule ya umma tunafaa kuwajibika kwa kuchunguza si kwa pekee matukio ya kipekee na athari za ubaguzi rangi, lakini pia ubaguzi wa rangi uliyoingia kitaasisi ambayo moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja imesababisha ubaguzi wa rangi na upendeleo katika sera na taratibu kadhaa za wilaya.

Katika kufuata ahadi yetu ya kuwajibika katika kushughulikia hatua ambazo hazikuchukuliwa awali ambazo kihistoria zimewatenga jamii zetu tofauti za masomo, tumeandaa itifaki mpya ya kuripoti tabia za ubaguzi (kama ubaguzi, unyanyasi, na ubaguzi wa rangi). Hii ni njia moja pekee katika kukabiliana na taratibu zisizo sawa katika wilaya yetu.

Katika wiki chache zijazo, tutafanya kazi kujenga ufahamu katika itifaki hiyo mpya ya kuripoti kwa wafanyikazi, wanafunzi, na familia ambazo zitakuwa na awamu kadhaa za vipindi vya **Kupinga Ubaguzi wa Rangi** ambazo wafanyikazi na wasimamizi watashiriki. Vipindi hivi vya mafunzo ya kupinga ubaguzi wa rangi vitaanza Novemba kwa wafanyikazi wote kote wilayani. Wakuu wa shule na wasimamizi wa ofisi ya kati wataendelea na mafunzo ya kimwezi kote mwaka wa shule wa 2020-21 huku timu ya wilaya ikipangia utekelezaji wa mpango wa kupinga ubaguzi wa rangi wa miaka kadhaa kote wilayani kuanzia mwaka ujao.

Tunaelewa kwamba kazi nyingi inahitajika kufanywa ili kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi katika Lowell, bila kujali rangi, ukoo, au hali ya kijamii na kiuchumi, anapata kwa usawa masomo ya hali ya juu ambayo itamsaidia kufikia uwezo wake wa juu zaidi. Tunakubali wajibu wetu kwa wanafunzi wetu na kwa jamii ya pana zaidi ya LPS wa kuandaa na kulinda mazingira ambapo wanafunzi wanahisi usalama, wanahisi wanaheshimiwa na wanahamasishwa. Ili kufikia huko, tunaendelea kujitolea kwa bidii za kusudi na zenye uendelevu katika kuimarisha sera na taratibu zetu za kutobagua, kutonyanyasa na kutobagua kirangi ili kuandaa mazingira ya masomo salama na yenye kukaribisha.

Kwa taarifa zaidi kuhusu itifaki yetu mpya, tafadhali tembelea tovuti letu la LPS na ubonyeze sehemu la [Ubaguzi, Unyanyasaji, na Ubaguzi wa Rangi](#) chini ya **Our District (Wilaya Yetu)** au wasiliana na Ofisi ya Usawa na Uimarishi katika (978) 674-4326. Kwa ziada, tafadhali tazama [ujumbe ya videyo](#) hii fupi inayohusiana na itifaki yetu mpya na kujitolea kwetu kwa usawa.

Wako Mwaminifu,

Dr. Joel D. Boyd
Msiamamizi Mkuu wa Mashule